

## 1. مَدُّ الصَّلَةِ الصُّغْرَى Maddusw-Swillatis-Sughraa:

Swillah ni kuunganisha herufi ya ه (haa) ya kiwakilishi<sup>1</sup> na herufi ya madd yenye kunasibiyana na *i'raab* yake (dhwammah au kasrah) kitakapokuwa hicho kiwakilishi cha ه ni chenye *i'raab* na kipo baina ya herufi mbili zenye *i'raab*. Swillah hii imegawanyika sehemu mbili mojawapo ni hii ya as-sughraa (ndogo) na ya pili yake ni ya al-kubraa (kubwa) itakayokuja maelezo yake katika Maddul-Far-'iy.

Mfano ya مَدُّ الصَّلَةِ الصُّغْرَى (Maddusw-swillatis-sughraa):

Tarjuma	Kutamkwa kwake	Mfano
Ambaye hutoa mali <b>yake</b> kwa ajili ya kujitakasa	مَا هُوَ ...maalahuw...	الَّذِي يُؤْتِي مَالَهُ 2 يَتْرَكِي
... Basi insani pale Mola wake Anapomtia mtihanini, Akamkirimisha (yeye) na Akamneemesha (yeye)...	رَبُّهُ فَكَّرَمَهُو وَنَعَّمَهُو ...Rabbuhuwa akramahuw wa na'-'amahuw...	فَأَمَّا الْإِنْسَانُ إِذَا مَا ابْتَلَاهُ رَبُّهُ فَكَّرَمَهُو 3 وَنَعَّمَهُو
Hakika <b>Yeye</b> kwa waja <b>Wake</b> ni ...	إِنَّهُ كَانَ بِعِبَادِهِي Innahuw kaana bi'ibaadihiy...	إِنَّهُ كَانَ بِعِبَادِهِ حَبِيرًا 4 بَصِيرًا

Sharti zake:

<sup>1</sup> ه (Haa) ya kiwakilishi ni nomino ya mwanamume ya mtu wa tatu (al-ghaaib) katika umoja (فرد) ambayo huwepo mwisho wa neno, yenye kuleta maana 'yeye' au 'yake'.

<sup>2</sup> Al-Layl (92: 18)

<sup>3</sup> Al-Fajr (89: 15)

<sup>4</sup> Al-Israa (17: 30, 96)

- i) Kuweko na *i'raab* (sio sukuwn au herufi ya madd) kabla ya ه (haa)
- ii) Kuweko na *i'raab* ifuatie katika neno la pili.
- iii) Haifuatwi na hamzah.

Zinapotimia sharti hizo, basi *i'raab* hizo hutamkwa kwa و (uw) au ي (iy) na kuvutwa kwake ni harakah mbili.

*Istithnaa* (Maneno yenye kwenda nje ya hukmu hii):

Maneno mawili pekee katika Qur-aan ambayo huwa hayafuati hukmu hii, kwa sababu ndivyo ilivyopokelewa kutoka riwaayah ya Hafsw 'an 'Aaswim *twariyq-Shaatwibiyyah*. Mojawapo ni kuvutwa kama inavyovutwa مَدُّ الصَّلَاةِ الصُّغْرَى (maddusw-swillatis-sughraa) japokuwa halina swiffah wala sharti za مَدُّ الصَّلَاةِ الصُّغْرَى (maddusw-swillatis-sughraa). La pili yake bila ya kuvutwa mvuto wa مَدُّ الصَّلَاةِ الصُّغْرَى (maddusw-swillatis-sughraa) huku likiwa na swiffah za sharti za مَدُّ الصَّلَاةِ الصُّغْرَى (maddusw-swillatis-sughraa). Nayo ni yafuatayo:

Hukmu haitimizwi		Hukmu inatimizwa	
<p>يَرْضَاهَاكُمْ ... yardhwahu lakum</p> <p>Bonyeza usikilize</p>	<p>وَإِنْ تَشْكُرُوا يَرْضَهُ لَكُمْ<sup>5</sup></p>	<p>فِيهِ ... fiyhiy muhaanah</p> <p>Bonyeza usikilize</p>	<p>وَيَخْلُدُ فِيهِ مُهَانًا<sup>6</sup></p>
<p>Haivutwi ه juu ya kuwa iko baina ya herufi mbili zenye <i>i'raab</i>.</p>		<p>Huvutwa ه juu ya kuwa herufi iliyoko kabla yake ni sukuwn.</p>	

<sup>5</sup> Az-Zumar (39 : 7)

<sup>6</sup> Al-Furqaan (25: 69)

